**MAADAMU YESU KRISTO YUPO KATIKATI YETU, HATA KAMA CHOMBO KINASUKWASUKWA NA UPEPO, BADO TUNA UHAKIKA WA KUWA SALAMA SAFARINI.**

**Maandiko: Mark. 4: 35 – 41, Sefan. 3: 15 – 17, na Waamuz. 6: 11 – 16**

1. **UTANGULIZI**
   **Ukisoma Biblia yote kwa makini sana, mojawapo ya jambo muhimu sana utakaloliona ni hili kwamba " Mungu tangu zamani amekuwa akitaabikia sana shida za wanadamu hata kama wanadamu walikuwa wamemkosea na hata kama wanadamu walikuwa wanamwazia Mungu kwa upumbavu.** Tangu alipomuumba Adamu na Hawa, akawaandalia na samaki na wanyama na matunda ya aina mbalimbali **!!!** ***Zab. 8:4-8, Mwz.1: 27-30, 2: 215- 17***, Mungu ni zaidi ya Baba zetu wa kimwili ambao walitutaabikia kipindi fulani tu kisha wakatuacha tujitaabikie sisi wenyewe; yeye anajitaabisha milele kwa ajili ya maisha yetu.
   - Aliwataabikia wana wa Israeli jangwani miaka 40!!! Hakuna Mwisrael aliyepanga bajeti ya maisha yake jangwani kwa miaka yote 40!!! Na hata waliojitahidi kuwa na mashaka na kumtilia shaka, kesho yake walimshangaa Mungu na wakaanza kutubu. ***Kut.16:11-35.***

2. **Lakini jambo lingine ambalo ukisoma Biblia kwa makini; utagundua kwamba wanadamu tangu zamani wana tabia ya kutaka kumlazimisha Mungu ili awaone kwamba wao hawafai, ni watoto wadogo, wanatoka katika familia maskini, hawajasoma na hawajui kusema!! Jambo ambalo Mungu hakubaliani nalo kabisa!!! Zab. 139: 13 – 14, Mwz. 1: 27, Kut. 4: 12, Yer. 1:4-10, Waam.6: 11-1 16**, n.k. Hili ni tatizo la wateule wengi hadi leo, ni wachache mno ambao **WAMEKUA** hadi kufika katika kiwango cha kukubali kuonekana kama Mungu anavyowaona!!!

- **Mungu ananiona kwamba ninafaa, ninaweza, ndiyo maana akaniokoa, akanichagua, akanitenga!!!**
- Tunashindwa kukabiliana na adui au hata mazingira tunayokutana nayo kwa sababu hii tu!! Tunajiona hatuwezi, hatufai, sisi ni wanyonge tu na tunajihukumu kabisa sisi wenyewe jambo ambalo linamfanya shetani atambe juu yetu na Mugu wetu kudhalilika. **Hes.13:26 – 33,** Hili limekuwa tatizo la kizazi hadi kizazi la kujiona kwamba hatufai, hatuwezi!! Ni wachache wanaofahamu kwamba wanaweza mambo yote maadamu Bwana yupo pamoja nao!!! ***Filip. 4: 13*; na wakati mwingine sisi wanadamu tunataka Mungu afanye mambo kama tunavyotaka sisi, na akifanya tofauti tunakasirika kabisa. *2Fal. 5: 9 – 12, (1Kor. 2: 12 – 14)*** Hili nalo ni tatizo kubwa sana kwa Kanisa la leo!!!

3. **Sasa tuje kwenye ujumbe wetu wa msingi siku ya leo kwamba "maadamu Bwana Yesu yupo katikati yetu (yupo pamoja nasi) hata kama chombo kinasukwasukwa na upepo mkali, bado tunayo hakika ya kuwa salama safarini!! *Mdo. 27: 14 – 38, 44.*** Huu ni uelewa ambao kila mteule anapaswa kuwa nao, hata katika misukosuko anayokutana nayo sasa afike mahala pa kugundua kama Yakobo kwamba" kumbe Bwana yupo pamoja nami. Mwz. 28: 16-22 na azame zaidi kwa kuelewa kuwa kama Bwana yupo katikati yake nini cha kumwogopesha?? ***Rum. 8:31 – 39;* tuache kuwa kama waigizaji tu ndugu zangu tunaponena kwamba tumeokoka; tufahamu kwamba sisi ndiyo tumepewa mamlaka na Mungu ya kunyamazisha dhoruba zinazovuma kwa sasa Tanzania na dunia kwa jumla**.
    - Mtumishi wa Mungu Paulo kwa kuwa alijitambua na akiwa katikati ya watu waliokuwa wamekata tamaa sababu ya dhiki na wanataka kujiua, alisimama na kutoa matamko na watu wote 276 wakaokoka na wakafika ng'ambo salama. **(je kama Paulo**

**asingesimama na kuwaambia maneno haya "Mdo.28: 22-25, sasa nawapeni shauri iweni na moyo mkuu, kwa maana hapana hata nafsi moja miongoni mwenu atakayepotea ila merikebu tu. Kwa maana usiku huu wa leo Malaika wa Mungu (Yesu) yule ambaye mimi ni wake, naye ndiye nimwabuduye, alisimama karibu nami, akaniambia, usiogope, Paulo, huna budi kusimama mbele ya Kaisaria, tena tazama, Mungu amekupa watu wote wanaosafiri pamoja nawe. Basi wanaume, changamkeni, kwasababu namwamini Mungu ya kwamba yatakuwa vile vile kama nilivyoambiwa na Mst. 44" nao waliosalia hawa juu ya mbao, na hawa juu ya vitu vingine vya maerikebu. Na hivyo watu wote wakapata kuifikilia nchi kavu salama**. Sisi ndiyo watuliza dhoruba, sisi ndiyo watuliza mionyo ya watu, sisi ndiyo tulio na majibu ya Watanzania!!! Sisi ndiyo watetezi wa Yesu Kristo katikati ya Manabii wa uongo na waalimu wa Uongo. ***1Wafa. 18: 21 – 40.***

- Hadi sasa Mungu anatungoja kwa hamu na anatutaka tuwe washirika katika kazi yake ya uumbaji na anachukizwa sana na mteule anayejiona kuwa ni mtoto na asiyeweza kufanya jambo lolote, ambaye ataendelea kukaa Kanisani bila ya kuwa na jukumu lolote la kufanya!!!

  **Note: Joshua alikuwa mwanadamu kama mimi na wewe na kwa sababu aliamini kwamba Bwana yupo pamoja na yeye, siku moja alitamka jambo kubwa na hakika Bwana akakubali litokee** – ***Josh. 10: 12-14***.

- Hii yote ni kwa sababu Yoshua ndani ya moyo wake aliona vyema amalize kabisa tatizo lililokuwa likiwatesa ndugu zake, akaona ni vyema jua lisimame hadi atakapomaliza vita ndipo aende akalale.

- Mungu akigundua kwamba mtumishi wake anatamka matamko Fulani kwa ajili ya kumdhibiti ibilisi na

kumpa Mungu utukufu mara zote matamko hayo anayaunga mkono soma. ***1Waf. 17: 1, 2Wafl. 7: 1 -2, Mdo. 3: 1- 10, 14: 8- 11.***

- Maana ya Mungu kuwa katikati yetu (kuwa pamoja nasi) ni Mungu anatutaka tuinuke na kutenda yatupasayo, Gidioni alipofahamu kwamba Bwana yupo pamoja naye, aliinuka na kisha akatenda yampasayo na akawa suluhisho la matatizo katikati a jamaa zake. ***Waam.7:19-25, 8:22-23.***

- Paulo pia alipogundua kwamba Mungu yupo pamoja naye hata kama walikuwa katikati wakati mgumu sana wa kukaa siku 14 bila kula chakula, alisimama na kuwatoa hofu wasafiri wote pamoja na nahodha na wote kweli wakaokoka kama tulivyosoma katika ***Mdo. 27: 21 -25, 44***

- **Nami nasimama leo kuwahakikishia wana wa Mungu kwamba, maadamu Bwana Yesu ni Yule Yule jana, leo na hata milele (*Ebr. 13: 8*) hata kama Nchi itakuwa na myumbo wa uchumi kwa sababu ya mabadiliko ya hali ya hewa au vita vya Urusi na Ukraine, bado watanzania tutaendelea kuwa salama; mvua zitanyesha za kutosha, magonjwa ya Ebola hayataingia katika Nchi yetu, Watanzania wasiwe na wasiwasi, Yuko Bwana Yesu mbadilisha majira na Nyakati wakati wote maana yeye nimweza wa Yoote. Amina**

***Na***
***Aksofu Dr. L. M.Mwizarubi.***
***16/Oct. 2022***